



JESHI LA ULINZI LA WANANCHI WA TANZANIA

Simu ya Upepo "N G O M E"
Simu ya Mdomo: "DOM + 255737962064"
Telex: "+255 (26) 2963757"
Fax: " + 255 262 962153"
Barua pepe: ulinzimagazine@tpdf.mil.tz
Tovuti: www.tpdf.mil.tz

Makao Makuu ya Jeshi,
Sanduku la Posta 194,
Dodoma, Tanzania
14 Aprili, 2026

NAFASI ZA KUANDIKISHWA JESHI

1. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linatangaza nafasi za kuandikishwa Jeshi kwa Vijana wa Kitanzania kuanzia elimu ya Sekondari hadi elimu ya Juu.
2. Vijana watakaoandikishwa Jeshi watapatiwa mafunzo mbalimbali muhimu ya Kijeshi na mafunzo ya kuwaendeleza katika taaluma zao.

SIFA ZA MWOMBAJI

3. Vijana wa Kitanzania wenye nia ya kuandikishwa Jeshi wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-
 - a. Awe Raia wa Tanzania wa kuzaliwa.
 - b. Awe na umri :-
 - (1) Usiozidi miaka 25 kwa elimu ya Kidato cha IV na Kidato cha VI.
 - (2) Usiozidi miaka 28 kwa elimu ya Juu.

f. Awe hajatumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo au chombo kingine chochote cha Ulinzi na Usalama.

g. Awe amehitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mkataba wa kujitolea miaka miwili (2) au Mujibu wa Sheria na kutunukiwa cheti.

UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

4. Maombi yote yaandikwe kwa mkono na yawasilishwe yalipokuwa Makao Makuu ya Jeshi Msalato Dodoma kuanzia tarehe 15 Aprili, 2026 hadi tarehe 28 Aprili, 2026 yakiwa na viambatisho vifuatavyo:-

- a. Nakala ya Kitambulisho cha Taifa au nambari ya NIDA.
- b. Nakala ya cheti cha kuzaliwa, vyeti vya Shule na Chuo.
- c. Nakala ya cheti cha JKT kwa waombaji waliomaliza mkataba. Aidha, Vijana waliopo kwenye Makambi ya JKT hawahusiki na tangazo hili.
- d. Nambari ya simu ya mkononi ya mwombaji.

MAOMBI YATUMWE KWA ANUANI IFUATAYO

Mkuu wa Utumishi Jeshini,
Makao Makuu ya Jeshi,
Sanduku la Posta 194,
DODOMA, Tanzania.

Imetolewa na

Baraka

Luteni Kanali Kevin Baraka Byabato
Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano
Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

